TANGAZO LA SERIKALI Na. 827 la tarehe. 4/10/2024

SHERIA YA USIMAMIZI WA HAKI NA MATUMIZI YA SHERIA,
(SURA YA 358)

---

# KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 4)*

KANUNI ZA UTEUZI, UJIRA NA NIDHAMU YA WASULUHISHI ZA MWAKA 2024

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina
2. Matumizi
3. Tafsiri

SEHEMU YA PILI
UTEUZI WA WASULUHISHI

4. Matumizi ya sehemu hii
5. Sifa za kuteuliwa kuwa Msuluhishi
6. Utaratibu wa Uteuzi
7. Uamuzi wa Maombi
8. Rejesta ya Wasuluhishi

SEHEMU YA TATU
UJIRA

9. Matumizi ya Sehemu hii
10. Ujira wa Wasuluhishi
11. Wajibu wa kulipa wasuluhishi

SEHEMU YA NNE
KANUNI ZA MAADILI NA HATUA ZA KINIDHAMU

12. Matumizi na Utekelezaji wa Kanuni za Maadili
13. Adhabu kwa kukiuka Kanuni za Maadili
14. Malalamiko kuhusu ukuikwaji wa maadili ya kitaaluma
15. Uchunguzi wa malalamiko

---

MAJEDWALI

---

SHERIA YA USIMAMIZI WA HAKI NA MATUMIZI YA SHERIA,
(SURA YA 358)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 4)*

KANUNI ZA UTEUZI, UJIRA NA NIDHAMU YA WASULUHISHI ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uteuzi, Ujira na Nidhamu ya Wasuluhishi za mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika kwa wasuluhishi wanaofanya usuluhishi ulioamriwa na mahakama au walioteuliwa kwa ajili hiyo.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Jaji Mfawidhi" maana yake ni Jaji Mfawidhi wa Masjala ya Mahakama Kuu, Masjala ndogo au Divisheni;

TS. Na. 148 la 2021

"Kanuni za Maadili" maana yake ni Kanuni za Maadili na Mwenendo wa Wapatanishi, Wasuluhishi na Waamuzi;

"ukiukaji wa maadili ya kitaaluma" maana yake ni kitendo chochote au kutotenda kunakochukuliwa kuwa ni ukiukaji wa Kanuni za Maadili; na

Sura ya 33

"usuluhishi ulioamriwa na mahakama" maana yake ni usuluhishi unaorejewa chini ya Amri ya Nane ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai.

## SEHEMU YA PILI
## UTEUZI WA WASULUHISHI

Matumizi ya Sehemu hii

**4**. Masharti ya Sehemu hii yatatumika kwa wasuluhishi ambao siyo maafisa wa mahakama wanaohudumu na waliostaafu.

Sifa za kuteuliwa kuwa msuluhishi TS. Na. 147 la 2021

**5**. Mtu atastahili kuteuliwa kuwa msuluhishi chini ya Kanuni hizi iwapo mtu huyo ameidhinishwa kuwa mpatanishi, msuluhishi au mwamuzi chini ya Kanuni za Uidhinishaji wa Watoa Huduma za Upatanishi, Usuluhishi na Uamuzi.

Utaratibu wa uteuzi

**6**.-(1) Mtu anayekusudia kuteuliwa kuwa msuluhishi atawasilisha maombi ya uteuzi kwa Jaji Mkuu.

(2) Maombi chini ya kanuni hii yatakuwa katika Fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na kuambatishwa na cheti cha uthibitisho kilichotolewa chini ya Kanuni za Uidhinishaji wa Watoa Huduma za Upatanishi, Usuluhishi na Uamuzi.

TS. Na. 147 ya 2021

Uamuzi wa maombi

**7**. Baada ya kupokea maombi, Jaji Mkuu, ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kupokelewa kwa maombi hayo-

(a) ikiwa ameridhika kwamba mwombaji anastahili kuteuliwa, atakubali maombi na kumjulisha mwombaji kwa maandishi kuhusu kuteuliwa kwake; au

(b) kama hajaridhika na maombi-

(i) atamtaka mwombaji kutoa maelezo zaidi kwa ajili kuzingatiwa; au

(ii) atakataa maombi na kumjulisha mwombaji kwa maandishi kuhusu kukataliwa huko na sababu zake.

Rejesta ya wasuluhishi

**8**. Msajili wa Mahakama Kuu atatunza rejesta ya wasuluhishi walioteuliwa chini ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TATU
## UJIRA

Matumizi ya Sehemu hii
Sura ya 33

**9**. Masharti ya Sehemu hii yatatumika kwa wasuluhishi wote isipokuwa msuluhishi aliyechaguliwa na wadaawa chini ya kanuni ya 25(6)(f) ya Amri ya Nane ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai.

Ujira wa wasuluhishi

**10**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sehemu hii, msuluhishi atastahili kulipwa ada ya huduma kwa kila shauri la upatanishi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Bila ya kuathiri kanuni ndogo ya (1), pale ambapo ni muhimu kwa msuluhishi kusafiri, atastahili kupata posho za safari na kujikimu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili:

Isipokuwa kwamba, pale ambapo msuluhishi ni afisa wa mahakama anayehudumu, gharama chini ya kanuni hii zitalipwa kwa mujibu wa masharti ya utumishi wake.

Wajibu wa kulipa wasuluhishi

**11**. Ujira, matumizi na gharama zinazopaswa kulipwa kwa msuluhishi chini ya Kanuni hizi zitalipwa na Mahakama.

## SEHEMU YA NNE
## KANUNI ZA MAADILI NA HATUA ZA KINIDHAMU

Matumizi na utekelezaji wa Kanuni za Maadili

**12**.-(1) Kanuni za Maadili zitatumika pamoja na mabadiliko muhimu yanayofaa kwa wasuluhishi chini ya Kanuni hizi.

(2) Jaji Mfawidhi atatekeleza Kanuni za Maadili kwa madhumuni ya kudhibiti nidhamu ya wasuluhishi.

(3) Msuluhishi anayekiuka Kanuni za Maadili anakiuka maadili ya kitaaluma.

Adhabu kwa kukiuka Kanuni za Maadili
Sura ya 237

**13**. Msuluhishi anayekiuka maadili ya kitaaluma-

(a) ikiwa ni afisa wa mahakama anayehudumu, atawajibika kwa hatua za kinidhamu kama ilivyoainishwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mahakama; au

(b) katika hali nyingine yoyote, atawajibika kwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Malalamiko kuhusu ukuikwaji wa maadili ya kitaaluma

**14**.-(1) Mtu ambaye hajaridhishwa na mwenendo wa msuluhishi na anaamini kuwa msuluhishi amekiuka maadili ya kitaaluma anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Jaji Mfawidhi dhidi ya ukiukwaji huo.

(2) Malalamiko yatafanyika kwa maandishi katika lugha ya Kiingereza au Kiswahili yakiungwa mkono na nyaraka nyingine yoyote au taarifa kama uthibitisho wa malalamiko hayo.

(3) Kanuni hizi hazitatafsiriwa kumzuia Jaji Mfawidhi kuanzisha mashauri ya kinidhamu kwa utashi wake.

Uchunguzi wa malalamiko

**15**.-(1) Jaji Mfawidhi, ndani ya siku saba baada ya kupokea malalamiko, ataamua kama malalamiko hayo ni ya msingi au ni uzushi na yasiyo na msingi.

(2) Endapo Jaji Mfawidhi ataridhika kwamba malalamiko ni ya msingi, kwa kuzingatia haki ya msuluhishi kusikilizwa, anaweza kutoa adhabu zifuatazo dhidi ya msuluhishi:

(a) kutoa onyo la maandishi;

(b) kumtaka kulipa kiasi cha fedha ambacho kinaweza kutosha kufidia gharama au hasara aliyopata mlalamikaji kutokana na malalamiko;

(c) kupendekeza kwa Jaji Mkuu kusimamishwa kazi au kutenguliwa kwa msuluhishi; au

(d) hatua nyingine yoyote kadri Jaji Mfawidhi atakavyoona inafaa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(2))*

FOMU MD

MAOMBI YA KUTEULIWA KUWA MSULUHISHI

…………………………………………………………………………………MWOMBAJI

1. Mimi………………………………………………………………………… (Anwani) naeleza kama ifuatavyo:
2. Kwamba, mwombaji ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyezaliwa tarehe ………………
3. Kwamba, mwombaji ameidhinishwa kuwa msuluhishi chini ya Kanuni za Uidhinishaji wa Watoa Huduma za Upatanisho, Majadiliano, Usuluhishi na Uamuzi za mwaka 2021 tarehe ………………
   Nakala za cheti cha kuzaliwa na cha uidhinishwaji vimeambatishwa pamoja na maombi haya .
4. Kwamba, uzoefu wa mwombaji kama msuluhishi uko katika (Bainisha maeneo ya utaalamu kwa mfano; Ardhi, uhamishaji miliki, ujenzi, kazi, bima, madini, mafuta na gesi n.k.): ……………………………… ……………………………………………………………………………………… …………………………………………………… ……………
5. Mwombaji anaomba ikupendeze kumteua kuwa msuluhishi chini ya kanuni ya 6(1) ya Kanuni za Uteuzi, Ujira na Nidhamu ya Wasuluhishi za mwaka 2024.

IMESAINIWA
Tarehe……......mwezi……………………..mwaka...................................

…………………
( MWOMBAJI)

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10)*

ADA NA POSHO
SEHEMU A:
ADA YA HUDUMA

| | MAAFISA WA MAHAKAMA WANAOHUDUMU | | WASULUHISHI TOFAUTI NA MAAFISA WA MAHAKAMA WANAOHUDUMU |
|---|---|---|---|
| Maelezo | | | Ada |
| Kwa kila usuluhishi uliofanikiwa. | Tshs. 500,000/= | | Tshs. 500,000/= |
| Kwa kila usuluhishi uliofanikiwa kwa sehemu. | Haitumiki | | Tshs. 300,000/= |
| Kwa kila usuluhishi usiofanikiwa. | Haitumiki | | Tshs. 200,000/= |

SEHEMU B:
POSHO YA USAFIRI NA KUJIKIMU

| S/N | AINA YA USAFIRI | DARAJA |
|---|---|---|
| 1 | Anga | Daraja la Uchumi |
| 2 | Bahari | Daraja la Kwanza |
| 3 | Treni | Daraja la Kwanza |
| 4 | Barabara | Daraja la kifahari |
| 5 | Ikiwa ni usafiri binafsi | Msuluhishi atastahiki posho ya mafuta kulingana na kiwango kinachotumiwa na Serikali |
| 6 | Posho ya kujikimu | Isiyozidi Tshs. 250,000/= kwa usiku |

Dodoma,
26 Septemba, 2024

IBRAHIM HAMIS JUMA,
*Jaji Mkuu*